**MUHTASARI WA KIKAO CHA DHARULA CHA BODI YA ZABUNI YA HALMASHAURI YA MJI NJOMBE KILICHOFANYIKA TAREHE 19/11/2021.**

**WALIOHUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Shigela Ganja | Kaimu Mwenyekiti |
| 2 | Zuhura Ahmadi | Katibu |
| 3 | Mtaka A.O | Mshauri |
| 4 | P.j. Mguli | Mjumbe |

**WASIOHUDHURIA**

1 . Thadei Luoga — Mwenyekiti

**SEKRETARIETI**

1 Elizabeth Kayani — Mwandishi — Sekretarieti

**MUHTASARI NAMBA 16.2021/2022. KUFUNGUA KIKAO**

16.1. Kikao kilifunguliwa na Mwenyekiti wa Bodi mnamo saa 08.44 Mchana.

16.2. Alianza kwa kuwashukuru wajumbe kwa mwitikio wao huku akiwataka kutoa michango yao katika hoja zilizopo mezani

**MUHTASARI NAMBA 17.2021/2022. KUPOKEA NA KUTHIBITISHA AGENDA**

17.1. Mwenyekiti aliwasomea wajumbe jumla ya agenda sita (6) zilizowasilishwa na kisha aliwauliza wajumbe kama wanazipokea.

17.2. Kwa pamoja wajumbe wote walikubali kwamba zijadiliwe kama zilivyo.

17.3. Agenda hizo ni kama ifuatavyo:

1 Kufungua kikao
2 Kuthibitisha Agenda.
2 Kuidhinisha utekelezaji wa fedha za miradi ya UVIKO 19
3 Mapendekezo ya kitengo cha manunuzi kuhusiana na majadiliano ya kitaalamu ya zabuni ya Ulinzi
4 Mapendekezo ya kitengo cha manunuzi kuhusiana na taarifa ya afisa maliasili kuhusu zabuni ya uuzaji wa miti ya pini shamba la njoomlole.
5 Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.
6 Kufunga kikao.

**MUHTASARI WA KIKAO CHA DHARULA CHA BODI YA ZABUNI YA HALMASHAURI YA MJI NJOMBE KILICHOFANYIKA TAREHE 19/11/2021.**

**WALIOHUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Shigela Ganja | Kaimu Mwenyekiti |
| 2 | Zuhura Ahmadi | Katibu |
| 3 | Mtaka A.O | Mshauri |
| 4 | P.j. Mguli | Mjumbe |

**WASIOHUDHURIA**

1 . Thadei Luoga — Mwenyekiti

**SEKRETARIETI**

1 Elizabeth Kayani — Mwandishi — Sekretarieti

**MUHTASARI NAMBA 16.2021/2022. KUFUNGUA KIKAO**

16.1. Kikao kilifunguliwa na Mwenyekiti wa Bodi mnamo saa 08.44 Mchana.

16.2. Alianza kwa kuwashukuru wajumbe kwa mwitikio wao huku akiwataka kutoa michango yao katika hoja zilizopo mezani

**MUHTASARI NAMBA 17.2021/2022. KUPOKEA NA KUTHIBITISHA AGENDA**

17.1. Mwenyekiti aliwasomea wajumbe jumla ya agenda sita (6) zilizowasilishwa na kisha aliwauliza wajumbe kama wanazipokea.

17.2. Kwa pamoja wajumbe wote walikubali kwamba zijadiliwe kama zilivyo.

17.3. Agenda hizo ni kama ifuatavyo:

1 Kufungua kikao
2 Kuthibitisha Agenda.
2 Kuidhinisha utekelezaji wa fedha za miradi ya UVIKO 19
3 Mapendekezo ya kitengo cha manunuzi kuhusiana na majadiliano ya kitaalamu ya zabuni ya Ulinzi
4 Mapendekezo ya kitengo cha manunuzi kuhusiana na taarifa ya afisa maliasili kuhusu zabuni ya uuzaji wa miti ya pini shamba la njoomlole.
5 Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.
6 Kufunga kikao.

**MUHTASARI NAMBA 18.2021/2022. KUIDHINISHA UTEKELEZAJI WA FEDHA ZA MIRADI YA UVIKO 19**

18.1 Katibu wa kikao aliwataarifu wajumbe kuwa halmashauri imepokea fedha kiasi cha tsh. 820,000,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya uviko 19 kwa mchanganuo ufuatao.

| NA | KATA | KIJIJI/KATA | JINA LA MRADI | KIASI CHA FEDHA KILICHO POKELEWA |
|---|---|---|---|---|
| 01 | Ihanga | Ihanga | Ujenzi wa madarasa 2 S/S ANNE MAKINDA | 40,000,000.00 |
| 02 | Ramadhani | Mpeto | Ujenzi wa madarasa 3 S/S Kibena | 60,000,000.00 |
| 03 | Kifanya | Kifanya | Ujenzi wa madarasa 4 S/S kifanya | 80,000,000.00 |
| 04 | Luponde | Lusitu | Ujenzi wa madarasa 2 s/s Luhololo | 40,000,000.00 |
| 05 | Njombe mji | Sido | Ujenzi wa madarasa 5 S/S Mabatini | 100,000,000.00 |
| 06 | Ramadhani | Maheve | Ujenzi wa madarasa 5 S/S Maheve | 100,000,000.00 |
| 07 | Matola | Matola | Ujenzi wa madarasa 4 S/S Matola | 80,000,000.00 |
| 08 | Lugenge | Lugenge | Ujenzi wa madarasa 2 S/S Mgola | 40,000,000.00 |
| 9 | Mjimwema | Mpechi | Ujenzi wa madarasa 5 S/S Mpechi | 100,000,000.00 |
| 10 | Iwungilo | Uliwa | Ujenzi wa madarasa 3 S/S Uliwa | 60,000,000.00 |
| 11 | Utalingolo | Utalingolo | Ujenzi wa darasa 1 S/S Utalingolo | 20,000,000.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 12 | Uwemba | Uwemba | Ujenzi wa darasa 1 S/S Uwemba | 20,000,000.00 |
| 13 | Ramadhani | Kibena Kati | Ujenzi wa bweni shule ya watoto wenye mahitaji maalumu kibena | 80,000,000.00 |
| JUMLA | | | | 820,000,000.00 |

18.2 Baada ya katibu kuwasilisha mchanganuo wa miradi, wajumbe walijadili na kukubaliana kwa pamoja kuwa miradi hiyo itekelezwe kwa "FORCE ACCOUNT" chini ya miongozo inayoelezeka. Hata hivyo mwenyekiti aliagiza katibu wa kikao kuhakikisha wote wanaotekeleza miradi hii wapewe barua zenye maelekezo ya namna utekelezaji wa miradi ikiwemo pamoja na kuwakumbushia taratibu za Manunuzi.

18.3 Aidha wajumbe walishauri kuwa miradi hii isimamiwe kwa ukaribu na waandisi pamoja na Idara husika ili kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa kufata vigezo na ubora unaotakiwa, Ikiwa sambamba na kukamilishwa kwa wakati.

**MUHTASARI NAMBA 19.2021/2022. MAPENDEKEZO YA KITENGO CHA MANUNUZI KUHUSIANA NA MAJADILIANO YA KITAALAMU YA ZABUNI YA ULINZI.**

19.1. Agenda hii iliwasilishwa na katibu wa bodi ya zabuni kufuatia kukamilika kwa kazi ya majadiliano ya timu ya wataalamu walioteuliwa na Halmashauri na Mzabuni aliyeitwa kwa ajili ya majadliano hayo.

19.2. Bodi ya zabuni iliyapitia mapendekezo ya timu ya majadiliano na Kitengo cha Manunuzi na kisha wajumbe kwa pamoja walilidhia zabuni ya ulinzi itanganzwe upya,pia mzabuni anaeendelea na kazi ya ulinzi bodi ya zabuni ililidhia aongezewe muda wa miezi mitatu hadi mchakato wa kumpata mzabuni mwingine ukamilike.

19.3 Pia wajumbe walishauri mkataba wa ulinzi uangaliwe vizuri kwani mzabuni anatekeleza kazi kwa matakwa yake na sio mkataba unavomuongoza, mwisho wajumbe walilidhia mchakato uendelee wa kutangaza

**MUHTASARI NAMBA 20.2021/2022. MAPENDEKEZO YA KITENGO CHA MANUNUZI KUHUSIANA NA TAARIFA YA AFISA MALIASILI KUHUSU ZABUNI YA UUZAJI MITI YA PINI SHAMBA LA NJOOMLOLE.**

20.1. Agenda hii iliwasilishwa na katibu wa bodi ya zabuni kufuatia kukamilika kwa tarifa ya msitu ambayo kikao cha bodi ya zabuni cha tarehe 7/10/2021 kiliagiza afisa maliasili alete taarifa ya msitu baada ya kuungua hali ipoje hadi sasa

20.2. Bodi ya zabuni iliyapitia mapendekezo ya Kitengo cha Manunuzi na kisha wajumbe kwa pamoja walilidhia zabuni ya uuzaji wa msitu itanganzwe upya,

**MUHTASARI NAMBA 21.2021/2022. MENGINEYO**

21.1. Kwa mujibu wa maelezo ya Mwenyekiti, ni kwamba hakukuwa na mengineyo yoyote yaliyowasilishwa mezani kwake.

**MUHTASARI NAMBA 22.2021/2022. KUFUNGA KIKAO.**

22.1. Wakati akiahirisha kikao, Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa ushiriki mzuri kwa muda wote wa kikao, alisisitiza kuendelea kufanya kazi kwa kuzingatia sheria, Kanuni na taratibu za manunuzi

22.2. Mwenyekiti aliahirisha kikao saa 09:00(saa tisa kamili) jioni.

**UMETHIBITISHWA**

................................ 
**KATIBU**

................................ 
**MWENYEKITI**

19/11/2021
................................ 
**TAREHE**

**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA MJI NJOMBE TAREHE 12/11/2021.**

**A. WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

1. Mhe. Erasto Mpete - Makamu Mwenyekiti wa H/Mji - Mwenyekiti
2. Mhe. Honolatus Mgaya - Mjumbe
3. Mhe. Catherine Mwalufuna - Mjumbe
4. Mhe. Ulrick Msemwa - Mjumbe
5. Mhe. Filoteus Mligo - Mjumbe

**B. WAJUMBE WASIOHUDHURIA:**

1. Mhe. Deodatus Mwanyika (Mb) - Mjumbe (kwa taarifa)

**C. MAAFISA TARAFA WALIOHUDHURIA:**

1. Ndg. Lilian Nyemele - Afisa Tarafa Njombe Mjini
2. Ndg. Tumaini Nganyagwa - Afisa Tarafa Igominyi

**D. WATAALAMU WALIOHUDHURIA:**

1. Ndg. Kuluthum Sadick - Mkurugenzi wa H/Mji - Katibu
2. Ndg. Consolata Mlowezi - Kny. Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala H/Mji
3. Ndg. Dorcas Mkello - Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara H/Mji
4. Ndg. Thadei Luoga - Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi H/Mji
5. Ndg. Shigela Ganja - Mkuu wa Idara ya Mipango Takwimu na Ufuatiliaji H/Mji
6. Dkt. Yesaya Mwasubila - Mkuu wa Idara ya Afya H/Mji
7. Ndg. Peter Magehema - Mratibu wa TASAF H/Mji
8. Mwl. Prochesius Mguli - Mkuu wa Idara ya Elimu ya Sekondari H/Mji
9. Mwl. Festo Salingwa - Kny: Mkuu wa Idara ya Elimu ya Msingi H/Mji
10. Ndg. Domitila Mwanyika - Kny. Mkuu wa Kitengo cha Nyuki H/Mji
11. Ndg. Isack Mapunda - Mkuu Kitengo cha TEHAMA H/Mji
12. Ndg. Upendo Mwamkemwa - Afisa Biashara H/Mji
13. Ndg. Emanuel Luhamba - Kny. Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili H/Mji
14. CPA. Joseph Sabule - Kny. Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani H/Mji
15. Ndg. Kenani Maliga - Kny. Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi H/Mji
16. Ndg. Hyasinta Kissima - Afisa Habari H/Mji
17. Ndg. Nelson Mlwisa - Kny. Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira H/Mji
18. Sr. Rogasiana Mwinuka - Kny. Mdhibiti wa Ubora wa Elimu H/Mji
19. Ndg. Christopher Henjewele - Katibu wa TSC H/Mji
20. Ndg. Ernest Ngaponda - Mkuu wa Idara ya Kilimo na Ushirika H/Mji
21. Ndg. Abdul Mtaka - Mkuu wa Kitengo cha Sheria H/Mji
22. Ndg. Zuhura Ahmad - Kny. Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi H/Mji
23. Ndg. Daniel Mwasongwe - Mratibu wa UKIMWI H/Mji
24. Eng. Bernadetha Mihambo - Kny. Mkuu wa Idara ya Ujenzi H/Mji
25. Ndg. Enembora Lema - Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii H/Mji
26. Ndg. Daniel Mbata - Kaimu Afisa Usafirishaji wa H/Mji
27. Ndg. Twilumba Mwalongo - Afisa Tawala H/Mji
28. Ndg. Deograsias Mkongwa - Mwandishi wa Vikao H/Mji
29. Ndg. Anthony Mtoni - Mwandishi wa Vikao H/Mji

**MUHTASARI NA.NTCK:F:U/VOL.4/46/2021/2022 – KUFUNGUA KIKAO**

46.1 Kabla ya kufungua kikao, Katibu aliwasalimia Wajumbe na kuwakaribisha kwenye kikao. Alieleza kuwa hiki ni kikao cha kawaida cha Kamati ya Fedha na Utawala na akidi ya Wajumbe imetimia hivyo alimkaribisha Mwenyekiti afungue kikao.

46.2 Mwenyekiti aliwasalimia Wajumbe na kuwakaribisha kwenye kikao. Aliwaomba Wajumbe kujadili agenda za kikao kwa kina.

46.3 Alifungua kikao saa 04:30 (saa nne na dakika thelathini) asubuhi.

**MUHTASARI NA.NTCK:F:U/VOL.4/47/2021/2022 – KUPOKEA AGENDA**

47.1 Agenda kumi (10) zilipokelewa na Wajumbe kama ifuatavyo:-

1. Kufungua Kikao.
2. Kupokea Agenda.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha na Utawala kilichofanyika tarehe 15/10/2021.
4. Yatokanayo na muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha na Utawala kilichofanyika tarehe 15/10/2021.
5. Taarifa ya Fedha (Mapato na Matumizi) inayoishia mwezi Oktoba, 2021.
6. Taarifa ya Mapato na Matumizi ya Mitambo ya Ujenzi inayoishia mwezi Oktoba, 2021
7. Taarifa ya Ukaguzi wa Ndani kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/2022 (Julai hadi Septemba, 2021)
8. Ombi la Kuidhinisha Fedha kwa Ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya UVICO 19
9. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.
10. Kuahirisha Kikao.

**MUHTASARI NA.NTCK:F:U/VOL.4/48/2021/2022 - KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA KILICHOFANYIKA TAREHE 15/10/2021.**

48.1 Muhtasari uliwasilishwa kwa Wajumbe na kufanyiwa masahihisho kama ifuatavyo:
- Dondoo Na. 33.1 neno kupiwa lisomeke kupewa
- Dondoo Na. 39.16 neno kuwa liondolewe

48.2 Mwenyekiti aliweka saini katika muhtasari na kuufanya kuwa moja ya kumbukumbu sahihi za Halmashauri.

**MUHTASARI NA.NTCK:F:U/VOL.4/49/2021/2022 - YATOKANAYO NA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA KILICHOFANYIKA TAREHE 15/10/2021.**

49.1 Dondoo Na. 37.9 kikao kiliagiza kuwa kwenye kikao kinachofuata, iwasilishwe taarifa ya ufuatiliaji wa kutambua sababu zilizosababisha kwa baadhi ya vizuizi kutokusanya mapato ya Halmashauri ukitolewa mfano wa kizuizi cha Mjimwema. Katika utekelezaji ilielezwa kuwa ufuatiiaji umefanyika katika vizuizi vyote ambavyo mapato hayakukusanywa. Hata hivyo katika vizuizi hivyo magari huwa hayapiti kila siku na hivyo kusababisha baadhi ya siku kutokusanya mapato japokuwa Msimamizi wa ukusanyaji wa mapato anakuwepo muda wote. Vizuizi vyenye hali hiyo ni pamoja na Mjimwema, Lunyanywi, Kisilo, Lugenge 1, Lugenge 2, Mgodechi, Utalingolo, Itulike na Yard ya Malori.

49.2 Wajumbe waliomba kufahamu kama bado kuna haja ya kujenga soko la mbao Kata ya Lugenge kwa kuwa vizuizi vya maeneo hayo magari hayapiti kila siku.

**Madhara**
Hesabu za mwisho za Halmashauri zinaweza kusababisha Hati chafu.

**Majibu ya menejimenti**
Tumepokea Ushauri wa Mkaguzi wa ndani tunaendelea kuufanyia kazi.

**Mapendekezo ya mkaguzi.**
Tunashauri marekebisho yafanyike kwa wakati.

**Maoni ya Kamati ya Fedha na Utawala.**

52.6 Wajumbe walishauri kuwa marekebisho katika taarifa ya hesabu za mwisho yafanyike mapema ili kuondoa hoja hiyo.

**5.2.5 Kuwepo kwa vifaa vya kuzuia majanga ya moto yanapotokea katika Jengo la Halmashauri ya Mji Njombe ambavyo vimeisha muda wa Matumizi.**
Wakati wa ukaguzi tuligundua kuwa Halmashauri ya Mji Njombe licha ya Kuwepo na mitungi ya kuzuia majanga ya moto pale yanapojitokeza lakini Mitungi hiyo maji yake yameisha muda wa matumizi yake ambapo muda wa Matumizi ulikuwa unaishia Mei 2021. Hii ni kwa mujibu wa sheria ya jeshi la zimamoto kifungu na.14 (427) ya mwaka 2007 na reg. 5 (1) ambayo inataka kuwepo na vifaa cha kuzuia moto endapo utatokea ili kulinda majengo yetu pamoja na mali mbalimbali.

**Ushauri.**
Tunashauri menejimenti ihakikishe kila wakati inajiridhisha kama vifaa vya kujikinga na majanga mbalimbali vinatunzwa katika hali inayokubalika kisheria kwa usalama wetu na mali zetu.

**Majibu ya Menejimenti**
Tumeanza hatua za manunuzi ili kuweza kufanyia kazi tatizo hili.

**Mapendekezo ya Mkaguzi.**
Tunasisitiza kuwa menejimenti ihakikishe inafuata sheria na kanuni zilizowekwa na Jeshi la zimamoto ili kuepuka majanga yanayosababishwa na moto.

**Maoni ya Kamati ya Fedha na Utawala**

52.7 Wajumbe walishauri kuwa vifaa vya kudhibiti majanga ya moto viwepo na viwe vinafanyiwa ukaguzi mara kwa mara. Hiyo itasaidia jengo la Halmashauri kuwa salama pindi likitokea janga la moto.

## MUHTASARI NA.NTCK:F:U/VOL.4/53/2021/2022 – OMBI LA KUIDHINISHIWA FEDHA KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA UVIKO 19

53.1 Ombi liliwasilishwa Kwa Wajumbe kama ifuatavyo;-

Ilitolewa taarifa kuwa Halmashauri ilipokea fedha kiasi cha Shilingi 820,000,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya uviko 19 kwa mchanganuo ufuatao.

| NA | KATA | KIJIJI/KATA | JINA LA MRADI | KIASI CHA FEDHA KILICHO POKELEWA |
|---|---|---|---|---|
| 01 | Ihanga | Ihanga | Ujenziwamadarasa 2 S/S ANNE MAKINDA | 40,000,000.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 02 | Ramadhani | Mpeto | Ujenziwamadarasa 3 S/S Kibena | 60,000,000.00 |
| 03 | Kifanya | Kifanya | Ujenziwamadarasa 4 S/S kifanya | 80,000,000.00 |
| 04 | Luponde | Lusitu | Ujenziwamadarasa 2 s/s Luhololo | 40,000,000.00 |
| 05 | Njombemji | Sido | Ujenziwamadarasa 5 S/S Mabatini | 100,000,000.00 |
| 06 | Ramadhani | Maheve | Ujenziwamadarasa 5 S/S Maheve | 100,000,000.00 |
| 07 | Matola | Matola | Ujenziwamadarasa 4 S/S Matola | 80,000,000.00 |
| 08 | Lugenge | Lugenge | Ujenziwamadarasa 2 S/S Mgola | 40,000,000.00 |
| 9 | Mjimwema | Mpechi | Ujenziwamadarasa 5 S/S Mpechi | 100,000,000.00 |
| 10 | Iwungilo | Uliwa | Ujenziwamadarasa 3 S/S Uliwa | 60,000,000.00 |
| 11 | Utalingolo | Utalingolo | Ujenziwadarasa 1 S/S Utalingolo | 20,000,000.00 |
| 12 | Uwemba | Uwemba | Ujenziwadarasa 1 S/S Uwemba | 20,000,000.00 |
| 13 | Ramadhani | Kibena Kati | Ujenziwabwenishuleyawatotoweny emahitajimaalumukibena | 80,000,000.00 |
| JUMLA | | | | 820,000,000.00 |

53.2 Wajumbe walilipokea ombi

**MAJADILIANO**

53.3 Wajumbe waliridhia ombi la utekekelezaji miradi ya UVICO 19 kutokana na fedha zilizoletwa.

53.4 Aidha Wajumbe walisisitiza kuwa wataalam wakazisimamie ipasavyo fedha hizo ili kuleta tija na ufanisi wa miradi hiyo.

**MUHTASARI NA.NTCK:F:U/VOL.4/54/2021/2022 – MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**

54.1 Hapakuwa na Mengineyo.

**MUHTASARI NA.NTCK:F:U/VOL.4/55/2021/2022 – KUAHIRISHA KIKAO**

55.1 Wakati akiahirisha kikao, Mwenyekiti aliwashukuru Wajumbe kwa kujadili agenda zote kwa kina na kusisitiza kuwa ukusanyaji wa mapato uzidi kuimarishwa. Makubaliano ya kikao yatekelezwe kama Wajumbe walivyokubaliana.

55.2 Aliahirisha kikao saa 07:03 (saa saba na dakika tatu) mchana.

…ARUHUSU USAMBAZWE:

SAINI: …[illegible]…

JINA: …KURUTHUM SADIK…
**KATIBU**

TAREHE: …10/12/2021…

MUHTASARI UMETHIBITISHWA:

SAINI: …[illegible]…

JINA: …ERASTO B. MPETE…
**MWENYEKITI**

TAREHE:…~~13~~ 14-12-2021…